**East African Journal of Swahili Studies**
eajss.eanso.org
**Volume 6, Issue 1, 2023**
**Print ISSN: 2707-3467 | Online ISSN: 2707-3475**
Title DOI: https://doi.org/10.37284/2707-3475

EAST AFRICAN NATURE & SCIENCE ORGANIZATION

*Original Article*

# Uchunguzi wa Mielekeo ya Walimu na Wanafunzi Kuhusu Mbinu na Nyenzo za Kufundishia Kiswahili Katika Shule za Upili za Umma, Kaunti za Kisumu na Kakamega, Kenya

*Linnah Apondi Okeyo[1*] Prof. John N. Kimemia, PhD[1] na Dkt. Sophia M. Ndethiu, PhD[1]*

[1] Chuo Kikuu cha Kenyatta, S. L. P. 43844-00100. Nairobi, Kenya
[*] Barua pepe ya mawasiliano: okeyo.linnah@gmail.com

**DOI ya Nakala: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1551**

**Tarehe ya Uchapishaji:**

*10 Novemba 2023*

**Istilahi Muhimu**:

*Mielekeo, Mbinu, Nyenzo, Kufundishia, Kiswahili na Matokeo.*

**IKISIRI**

Utafiti huu ulichunguza mielekeo ya walimu na wanafunzi kuhusu mbinu na nyenzo zlizotumiwa wakati wa kufunza Kiswahili katika shule za upili katika Kaunti za Kisumu na Kakamega nchini. Lengo la utafiti huu lilikuwa kutambua mbinu na nyenzo zilizotumiwa na walimu pamoja na wanafunzi wao kufunza na kujifunza Kiswahili pamoja na mielekeo yao kuzihusu.Utafiti ulilenga idadi ya walimu na wakuu wa idara 12 katika kila Kaunti pamoja na wanafunzi 960. Data ilikusanywa kupitia hojaji za wanafunzi na walimu, mwongozo wa usaili kwa wakuu wa Idara ya Kiswahili pamoja na uchunguzi wa darasani. Data zilichanganuliwa kwa kutumia Toleo la takwimu 13 kuonyesha idadi katika alama za asilimia na uradidi.Mbinu walizochangamkia wanafunzi masimulizi, mihadhara na maonyesho) sizo zilizotumiwa na walimu kila mara kuwafunza. Mbinu za kikoa, na mseto pamoja na usomaji mpana na wa kina (vitabu vya ziada, viteule na gazeti la Taifa Leo) zilitumika sana Kakamega hali iliyochangia matokeo yao kuwa bora kiasi kuliko ya Kisumu. Mbinu za jadi zilichangamkiwa zaidi katika kaunti zote madjhali mbinu za kidijitali hazikutumiwa sana.Ilibainika kuwa pana uhusiano kati ya mielekeo, utendakazi na matokeo ya wanafunzi somoni; mielekeo chanya iliathiri utendakazi na matokeo kwa namna chanya bali mielekeo hasi ikiathiri haya yote kwa namna hasi. Walimu waboreshe mbnu na nyenzo wanazozitumia kufunza Kiswahili ili matokeo yake yapate kuimarika zaidi katika shule zote, kaunti zote na nchini.

**APA CITATION**

Okeyo, L. A., Kimemia, J. N. & Ndethiu, S. M. (2023). Uchunguzi wa Mielekeo ya Walimu na Wanafunzi Kuhusu Mbinu na Nyenzo za Kufundishia Kiswahili Katika Shule za Upili za Umma, Kaunti za Kisumu na Kakamega, Kenya. *East African Journal of Swahili Studies*, *6*(1), 448-467. https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1551.

**CHICAGO CITATION**

Okeyo, Linnah Apondi, John N. Kimemia and Sophia M. Ndethiu. 2023. “Uchunguzi wa Mielekeo ya Walimu na Wanafunzi Kuhusu Mbinu na Nyenzo za Kufundishia Kiswahili Katika Shule za Upili za Umma, Kaunti za Kisumu na Kakamega, Kenya”. *East African Journal of Swahili Studies* 6 (1), 448-467. https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1551.

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

East African Journal of Swahili Studies, Volume 6, Issue 1, 2023
Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1551

**HARVARD CITATION**
Okeyo, L. A., Kimemia, J. N. & Ndethiu, S. M. (2023) "Uchunguzi wa Mielekeo ya Walimu na Wanafunzi Kuhusu Mbinu na Nyenzo za Kufundishia Kiswahili Katika Shule za Upili za Umma, Kaunti za Kisumu na Kakamega, Kenya", *East African Journal of Swahili Studies*, 6(1), pp. 448-467. doi: 10.37284/jammk.6.1.1551.

**IEEE CITATION**
L. A. Okeyo, J. N. Kimemia & S. M. Ndethiu "Uchunguzi wa Mielekeo ya Walimu na Wanafunzi Kuhusu Mbinu na Nyenzo za Kufundishia Kiswahili Katika Shule za Upili za Umma, Kaunti za Kisumu na Kakamega, Kenya", *EAJSS*, vol. 6, no. 1, pp. 448-467, Nov. 2023.

**MLA CITATION**
Okeyo, Linnah Apondi, John N. Kimemia & Sophia M. Ndethiu. "Uchunguzi wa Mielekeo ya Walimu na Wanafunzi Kuhusu Mbinu na Nyenzo za Kufundishia Kiswahili Katika Shule za Upili za Umma, Kaunti za Kisumu na Kakamega, Kenya". *East African Journal of Swahili Studies*, Vol. 6, no. 1, Nov. 2023, pp. 448-467, doi:10.37284/jammk.6.1.1551.

## UTANGULIZI

Lugha ni kipengee muhimu katika kukuza mawasiliano, kupanua fikra na kubadilishana mawazo, fikra, jumbe, hisia na mielekeo miongoni mwa waja (Aziz, 2003). Kwa kawaida, mitazamo ya walimu na wanafunzi kuhusu tajriba zao na maarifa yao ya awali huathiri ufunzaji na ujifunzaji wao. Lugha huathiri anavyofikiria mtu na kujieleza hivyo mielekeo ya walimu na wanfunzi kuhusu lugha ya Kiswahili huweza kuwa na mchango mkubwa katika kufanikisha shughuli ya ufunzaji na ujifunzaji wao (Adeyemo, 2011).

Kiswahili ni somo la lazima katika shule za msingi na upili. Hii ni kutokana na dhima na umuhimu wake hapa nchini Kenya. Hii ndiyo lugha ya taifa letu iliyotambulika kuwa na uwezo wa kuleta umoja wa kitaifa. Fauka ya haya, Kiswahili si lugha ya tabaka au kabila moja bali ni lugha ambayo kila mtu wa kila kabila na rika katika taifa zima anaweza akadai kuwa ni yake. Ingawa Kiswahili ni somo la lazima katika shule za upili nchini, sera za lugha katika shule nyingi huathiri sana matumizi ya lugha shuleni na hatimaye kuchangia katika kuwepo kwa mielekeo mbalimbali kuhusu lugha ya Kiswahili. Utafiti huu ulijikita zaidi katika mielekeo ya wanafunzi, na walimu wa Kiswahili kuhusu ufunzaji na ujifunzaji wake katika shule za upili nchini. Wanafunzi na walimu wana ushawishi mkubwa sana kutokana na nafasi yao katika jamii. Wote wanaheshimika na kuenziwa; walimu kutokana na mamlaka waliyopewa na maarifa waliyonayo, wanafunzi nao ni kwa sababu ya nafasi yao masomoni. Kutokana na ukweli huo, tabia na mienendo yao, pamoja na matamshi yao mbalimbali yana athari kubwa sana katika jamii. Mara nyingi, watu wengi hupenda kuiga wayafanyayo; hali inayobainika hasa katika matumizi yao ya lugha kimaongezi na kimaandishi.

Kwa mujibu wa Onyango (2008) mielekeo ni hisia zinazomfanya mtu ajenge mitazamo au imani fulani kuhusu vitu, watu au jambo fulani katika mazingira au jamii yake. Mielekeo mizuri au ile chanya humfanya mtu akakipenda kitu ilhali mielekeo mibaya au ile hasi humfanya akakichukia. Aghalabu, mielekeo ya wanafunzi kuhusu mwalimu wao husababishwa na mambo yafuatayo:

- Mbinu ambazo mwalimu hutumia kufundishia mada za Kiswahili; wanafunzi wanaweza kuzipenda au kuzichukia.
- Ufasaha wa mwalimu huyo katika lugha ya pili anayofundisha; umilisi na utendaji wake katika Kiswahili.
- Mwelekeo wa mwalimu mwenyewe kuhusu lugha ya pili. Ikiwa anaichukia lugha hiyo kinyume kabisa na matarajio ya wanafunzi wake, basi wanaweza kumchukia.
- Adhabu ambazo mwalimu huyo huwapa wanafunzi.Mwalimu anayependa kuwaadhibu wanafunzi wake wanapofanya makosa anaweza kuwaogofya wanafunzi hao kuuliza au kujibu maswali darasani au hata kuzungumza naye nje ya darasa. Hali kama hii huweza kuathiri sana uwezo wa wanafunzi

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1551

hawa kuimudu, kithamini na kuitumia lugha yenyewe kikamilifu.

Mielekeo ya walimu huchukuliwa kuwa na nafasi kubwa katika kuwafunza wanafunzi madarasani. Walimu hufanya maamuzi kuhusu maingiliano darasani kulingana na mielekeo yao kuhusu kufunza na kujifunza. Cummin na Lindsey (2004) wanashikilia kuwa kila anachofanya mwalimu hudhihirisha yale ambayo anayafahamu, anayaamini na kuwa maarifa ya mwalimu pamoja na anavyowaza hubainisha msingi wa kipekee unaotawala matendo yake akiwa darasani. Utafiti huonyesha kuwa kuna mchango wa mwalimu katika kukuza matokeo ya wanafunzi pasi na kujali viwango vyake katika elimu na mazingira yake ya kinyumbani. Kwa hakika, utafiti umeonyesha kuwa mielekeo ya walimu ni jambo la kimsingi sana katika kutabiri matokeo ya mwanafunzi kimasomo (Adeyemo, 2011). Utafiti huu ulilenga kuchunguza mchango wa mielekeo ya walimu na wanafunzi kuhusu lugha ya Kiswahili katika ufunzaji na ujifunzaji wake katika shule za upili.

## Lengo la Utafiti

Kuchunguza mielekeo ya walimu na wanafunzi ilivyoathiri shughuli za kufunza na kujifunza lugha ya Kiswahili katika shule za upili katika Kaunti za Kakamega na Kisumu nchini Kenya.

## Umuhimu wa Utafiti

Kulingana na matokeo ya wanafunzi katika mtihani wa Kiswahili wa KCSE tangu utahini wa Kiswahili ubadilishwe mwaka wa 2006, ni dhahiri kuwa somo hili halijakuwa likifanywa vyema kitaifa. Kwa sababu ya hali hii, palikuwa na haja kuu ya kubainisha vyanzo vya matokeo haya duni kwa kuzingatia mielekeo ya walimu na wanafunzi kwa kuzingatia mbinu na nyenzo mbalimbali na athari zake katika ufunzaji na ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili nchini Kenya. Matokeo ya wanafunzi katika somo lolote lile huweza kulingana na hali ilivyo kijamii, kiuchumi, kisaikolojia na kimazingira. Hata hivyo, jambo la kimsingi katika shughuli nzima ya kufunza na kujifunza ni hali ya wahusika kisaikolojia. Isitoshe, tafiti nyingi ulimwenguni zimeonyesha kuwa njia za kufunza huwa na mchango mkubwa sana katika matokeo ya wanafunzi hivyo basi palikuwa na haja ya kuelewa jinsi ambavyo mielekeo ya walimu na wanafunzi wa shule za upili huweza kuathiri njia za kufunza lugha na hatimaye kujifunza kwake unaobainika katika matokeo ya wanafunzi.

## YALIYOANDIKWA KUHUSU MADA

Kwa mujibu wa Onyango (2008) mielekeo ni hisia zinazomfanya mtu ajenge mitazamo au imani fulani kuhusu vitu, watu au jambo fulani katika mazingira au jamii yake. Mielekeo mizuri au ile chanya humfanya mtu akakipenda kitu ilhali mielekeo mibaya au ile hasi humfanya akakichukia. Kwa mujibu wa Stitt-Gohdes (2001), Henson (2004) na Hou (2007) mbinu za kufunza na kujifunza huboresha na kuimarisha matokeo ya wanafunzi. Kufunza kuzuri ni kule kunakosababisha na kukuza ujifunzaji. Umuhimu wa mbinu mwafaka katika ufundishaji wa Kiswahili unaungwa mkono na wataalamu wengi (Ellis, 1997; Lighbown na Spada, 1990; Gathumbi na Masembe, 2005). Mbinu au njia za kufunza zenye manufaa makubwa kwa wanafunzi ni zile zinazohusisha ushirikisho wao. Mbinu za ufundishaji ni kigezo muhimu katika ufundishaji na kuboresha stadi za lugha ya Kiswahili; kusikiliza, kuongea, kusoma na kuandika. Kulingana na Chika 2012, kujifunza hufaulu zaidi wanafunzi wanapohusishwa katika mambo yote yanayotendeka madarasani kwa kuuliza maswali na kutawala maongezi. Ufundishaji mwafaka hutegemea mbinu zinazoweza kushirikisha wanafunzi katika kutoa maoni yao darasani ili kukuza uwezo wao wa kuwasiliana kwa ukakamavu na ufasaha. Mbinu zinazotumiwa kufundishia lugha hutegemea vigezo kama; mada inayofunzwa, umri wa wanafunzi, kiwango cha uelewaji wao, madhumuni na stadi husika, ujuzi wa mwalimu, tajriba yake na mbinu za kuwaelekeza wanafunzi darasani (Magare, 2017). Wengi wa walimu hubuni njia za kufunza kutegemea imani yao kuhusu yanayochukuliwa kama kufunza ambako ni bora, uwezo wao

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

pamoja na itikadi za kawaida katika kila taaluma (Watson, 2003).

Kuna baadhi ya walimu wanaoamini kuwa wao ndio wanaostahili kutawala na kuwapa maagizo wanafunzi. Wao hushikilia kuwa mwalimu ndiye nguzo kuu katika kufunza kwa kuwa ndiye mjuzi na mtaalam katika mada inayozingatiwa. Hata hivyo, kuna walimu wanaoamini kuwa mwanafunzi ndiye anayestahili kuwa kigezo muhimu huku mwalimu akiwa mwelekezi au hata mwongozo wake anapojifunza (Ahmad na Aziz, 2009). Kutokana na madai haya palikuwa na haja ya kutambua jinsi mambo yalivyo katika madarasa ya lugha ya Kiswahili katika kaunti za Kisumu na Kakamega.

Kwa mujibu wa Cannon na Palmiter (2003), ni wazi kuwa madarasa ambayo zawadi na himizo hutolewa na kutumiwa, wanafunzi huwa na mielekeo iliyo chanya zaidi na hufanya vyema kuliko wale wa madarasa ambayo zawadi na himizo hukosekana na mitazamo yao pia haitiliwi maanani katika ufunzaji na ujifunzaji. Hii ni kwa kuwa zawadi na himizo huweza kumchochea mwanafunzi kutaka kuchangia na kushiriki vilivyo katika shughuli nzima ya ufunzaji na ujifunzaji.

Isitoshe, inaakisiwa kuwa ujifunzaji na motisha ya wanafunzi hutambuliwa kwa kiwango kikubwa na mielekeo yao; na hata zaidi kuliko nia za mwalimu au mielekeo yake. Maarifa kuhusu mielekeo ya wanafunzi ni muhimu kwa walimu kukadiria inavyoathiri tabia za wanafunzi hao. Kutokana na hali kuwa kuna uhusiano mkubwa kati ya mielekeo ya wanafunzi katika matokeo yao, mielekeo hiyo inaweza kuwa na ushahidi wa kutosha wa namna inavyoathiri ujifunzaji kuliko mielekeo ya walimu au hata watazamaji wengine (Adeyemo, 2011). Utafiti huu ulinuia kuthibitisha madai haya pamoja na kuchunguza iwapo kulikuwa na uhusiano kati ya mielekeo ya walimu na utendakazi wao pamoja na matokeo ya wanafunzi wao. Fauka ya hayo, si wazi iwapo walimu wanaofunza lugha hufunza kulingana na imani yao au wao huongozwa na mambo mengine. Isitoshe, mikakati inayotumiwa kufunza na kujifunza lugha ni jambo linalohitaji uchambuzi kwani haitambuliki waziwazi. Utafiti huu ulilenga kuziba hili pengo lililoonekana kuwepo katika nyanja za tafiti kuhusu ufunzaji na ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili shuleni upili.

Kulingana na silabasi ya sasa (KIE, 2002), mada zote za Kiswahili zinastahili kusetwa; kufunza pale ambapo mada kutoka sehemu mbalimbali katika somo hili hufunzwa kwa pamoja katika kipindi kimoja darasani (Otunga na wenzake, 2011). Mbinu ya mseto katika ufunzaji wa Kiswahili ina maana kuwa stadi za lugha; kusikiliza, kusoma, kuandika na kuongea pamoja na sarufi na matumizi ya lugha hazipokezwi kwa njia iliyotengwa bali hufunzwa yote kitaratibu katika kipindi kimoja ili kutosheleza na kufanikisha kila moja yao na nyingine (KIE, 2002; Otunga na wenzake, 2011). Ufunzaji kupitia njia ya kusetwa kwa mada mbalimbali ni utaratibu wenye manufaa zaidi kwa kuwa mwanafunzi hupata muda mzuri wa kuelewa mada zinazofunzwa vyema zaidi. Isitoshe, ni njia inayomwezesha mwanafunzi kujifunza kwa ukamilifu. Mbinu hii ya mseto huzingatiwa katika viwango mbalimbali ambavyo ni bainifu (KIE 2002). Utafiti huu ulilenga kubaini hali ilivyo katika madarasa ya Kiswahili kulingana na mikakati inayotumiwa na walimu wa somo hili kufanikisha ufunzaji na ujifunzaji wake.

Mifumo ya kielimu kote nchini ina shinikizo kuu la kuseta mfumo wa kidijitali katika ufunzaji na ujifunzaji wa masomo yote katika mitaala na Kenya haijaachwa nyuma. Kenya kama taifa imesisitiza umuhimu wa mbinu hii ya kidijitali katika shughuli za ufunzaji na ujifunzaji kupitia programu za kuinua elimu nchini (KESSP). Hii inadhihirika kupitia uanzilishaji wa mikakati ya elimu na ufunzaji stadi kitaifa ya ICT (MOE, 2005). Njia hii itaiwezesha kutimiza ndoto yake ya kuhakikisha wote wamepata elimu (EFA) pamoja na kutimiza malengo ya milenia (MDGs).

Walimu wa Kiswahili kama wale wa lugha nyinginezo hutumia njia za jadi pamoja na za kisasa kufanikisha ufunzaji wao. Njia za jadi za kufunza hujumuisha matumizi ya chaki na ubao, vitabu vya kusoma, chati, redio na televisheni. Kulingana na Look (2005), teknolojia ya kisasa

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1551

hurejelea matumizi ya programu za tarakilishi kufunzia masomo mbalimbali. Nchini, walimu katika viwango vyote wameandaliwa na kuhimizwa kutumia njia za kidijitali katika shughuli za ufunzaji na ujifunzaji ili kutimiza malengo yao na kuinua viwango vya elimu; walimu wa Kiswahili hawajaachwa nyuma. Matumizi ya tarakilishi na mtandao au intaneti huweza kutumika kutoa jumbe zinazoweza kuinua na kuboresha shughuli za ufunzaji na ujifunzaji (Guha, 2003).

## MBINU ZA UTAFITI

Muundo wa kisoroveya hulenga kumwezesha mtafiti kuelezea mielekeo, maoni, tabia na sifa za jumuiya nzima kwa kutumia data inayotokana na sampuli itakayoteuliwa (Creswell, 2014). Utafiti huu ulifuata utaratibu au muundo wa kisoroveya na wa ulinganuzi. Jumuiya lengwa ya utafiti huu ilikuwa walimu waliofunza somo la Kiswahili katika kidato cha tatu na wanafunzi wa kidato cha tatu katika shule za upili katika kaunti za Kisumu na Kakamega. Jumuiya finyu iliyohusisha shule 24 iliteuliwa kupitia sampuli kusudio, kila kaunti iliwakilishwa na shule 12. Baadaye, shule 6 katika kila kaunti ziliteuliwa kinasibu kutoka kwenye kundi maalum la shule zilizopatikana mijini na zilizoko vijijini huku jumuiya finyu ya wanafunzi wa kidato cha 3 iliteuliwa kutoka kila shule. Shule zilizoteuliwa ziliwekwa katika makundi kuhakikisha kuwa katika kila kaunti na eneo shule mbili mbili za jinsia moja; za kike na za kiume na mbili za mseto ziliteuliwa.Ni kutokana na jumuiya finyu hii ya jumla ya shule 24 za upili na wanafunzi kutoka mkondo mmoja wa kidato cha tatu katika kila shule iliyoteuliwa kinasibu ambapo sampuli ya utafiti huu ilichaguliwa. Shule zilizokuwa na mkondo mmoja tu katika kidato cha tatu darasa hilo liliteuliwa kupitia utaratibu wa kimakusudi hivyo wanafunzi 969 walijumuishwa katika utafiti huu. Walimu wa Kiswahili 24 waliofunza madarasa yaliyochaguliwa pamoja na walimu walioongoza shughuli za idara ya Kiswahili 24 katika shule zilizoteuliwa; walihusishwa katika utafiti huu kimaksudi. Mtafiti alitumia mahojiano, hojaji, mtihani wa insha ya kiubunifu na mitazamo ya darasani katika ukusanyaji wa data. Data ya utafiti huu ilichanganuliwa kwa kutumia program ya uchunguzi wa toleo la takwimu 13 na iliwasilishwa kwa njia ya kijarabati kutumia michoro na majedwali.

## MATOKEO

Mbinu za kufunzia zilikadiriwa na wanafunzi kupitia majibu kwenye hojaji zao kuwa zinaridhisha sana Kakamega kwa asilimia 68 ($n$ = 387) na 61.4 ($n$ = 245) katika kaunti ya Kisumu na kuwa haziridhishi kwa asilimia 6.3 ($n$ = 36) Kakamega na 8.8 ($n$ = 35) Kisumu. Kijumla, wanafunzi 632 (65.3%) walishikilia kuwa mbinu walizozitumia walimu kuwafunzia zilikuwa za kuridhisha sana. Hii inaashiria kuwa wanafunzi walikuwa na mielekeo chanya kuhusu mbinu za kufunzia zilizotumiwa na walimu wao. Mbinu ya kidijitali ilikadiriwa kutotumiwa sana katika kaunti ya Kakamega kuliko hali ilivyokuwa katika kaunti ya Kisumu kwa aslimia 65.8 ($n$ = 374) na 65.2 ($n$ = 260), mtawalia. Mbinu za kidijitali zilitambuliwa na wanafunzi wengi 634(65.6%) kuwa hazikutumiwa na walimu wao kuwafunza Kiswahili japo wanafunzi 242 (25.1%) walikubali kuwa walimu wao walihusisha mbinu hii walipowafunza. Matokeo haya yanawiana na maoni ya Miima (2014) kuwa walimu wachache tu ndio waliotumia vifaa vya kidijitali kufunzia lugha ya Kiswahili, wengi wao walifurahia na kuridhika kutumia mbinu za kijadi (kitamaduni) au za kawaida kufunzia.

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1551

**Jedwali 1: Maoni ya wanafunzi kuhusu mbinu na vifaa vya kufunzia**

| Mbinu Za Kufunzia | Inatumika | | | | Haitumiki | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | KAKAMEGA | | KISUMU | | KAKAMEGA | | KISUMU | |
| | % | n | % | n | % | n | % | n |
| Mihadhara | 64.8 | 365 | 54.6 | 212 | 35.2 | 198 | 45.4 | 178 |
| Maonyesho | 33.5 | 189 | 38.5 | 153 | 66.5 | 376 | 61.6 | 245 |
| Majadiliano | 89.1 | 505 | 83.6 | 332 | 10.9 | 62 | 16.4 | 65 |
| Maswali na majibu | 94.2 | 533 | 90.2 | 360 | 5.8 | 33 | 9.8 | 39 |
| Masimulizi | 74.4 | 418 | 70.1 | 279 | 25.6 | 144 | 29.9 | 119 |
| Mbinu ya kikoa | 79.1 | 447 | 81.4 | 323 | 20.9 | 118 | 18.6 | 74 |
| Mbinu za kidijitali | 24.7 | 140 | 25.5 | 102 | 65.8 | 374 | 65.2 | 260 |
| Mbinu mseto | 36.2 | 206 | 37.4 | 149 | 45.1 | 257 | 47.1 | 188 |
| NYENZO | | | | | | | | |
| Kiswahili kitukuzwe | 88.9 | 507 | 87.7 | 350 | 10.1 | 63 | 12.4 | 49 |
| Mbinu kuridhisha | 68 | 387 | 61.4 | 245 | 6.3 | 36 | 8.8 | 35 |

Kuhusu mada kusetwa darasani, ilibainika wazi kuwa mbinu hii haikutumika sana kufunzia Kiswahili (Rejelea *Jedwali 1*). Maoni haya yanawiana na ya Opunde (Haijulikani) aliyebainisha kuwa mwelekeo mseto katika ufundishaji wa lugha si dhana mpya katika mitaala ya elimu nchini Kenya ilhali utekelezwaji wake katika ufundishaji wa Kiswahili bado ni changamano. Rutere (2012) aliunga maoni haya kuwa usetaji huhitaji muda mwingi wakati wa maandalizi na utendakazi hivyo hauzingatiwi na walimu wengi. Pia, mbinu ya kikoa ilibainika kutumiwa sana Kisumu kwa asilimia 81.4 ($n$ = 323) na Kakamega kwa asilimia 79.1 ($n$ = 447). Kwa jumla, wanafunzi wengi 770 (80%) walikubali kuwa walimu wao walitumia mbinu ya kikoa kuwafunza somo la Kiswahili kudhihirisha kuwa mbinu hii ilitumika sana. Matokeo haya yanadhihirisha kuwa walimu walithamini sana ushirika katika utendakazi wao hivyo kuinuana na kuwafaidi wanafunzi wao kwa njia mbalimbali.

Kwa mujibu wa wanafunzi, mbinu iliyotumiwa zaidi na walimu wao ilikuwa maswali na majibu ikifuatwa na majadiliano na masimulizi huku mihadhara na maonyesho ikibainika kutumika kwa nadra sana. Hata hivyo, mbinu hizo zilikadiriwa kutumika sana Kakamega kuliko zilivyotumika Kisumu isipokuwa mbinu ya maonyesho iliyotumika sana Kisumu kushinda Kakamega. Mbinu shirikishi zilitumika sana Kakamega kuliko hali ilivyokuwa Kisumu jambo ambalo huenda lilichangia katika kuimarisha umilisi na utendaji wa wanafunzi katika somo la Kiswahili kama ilivyodokezwa katika matokeo ya mtihani wa Insha ya ubunifu. Matokeo haya yanalingana na maoni ya Mukwana na Too (2014) waliosisitiza kuwa mbinu ambazo hazimhusishi mwanafunzi si bora kwa kuwa wanafunzi huachwa nje ya mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji wa somo kutokana na hali kuwa mwalimu ndiye huchukua usukani.

Katika kaunti ya Kakamega, ilidhihirika kuwa asilimia 68 ($n$ = 387) waliridhika sana na mbinu zao za kujifunza bali asilimia 6.3 ($n$ = 36) hawakuridhika. Kisumu, asilimia 61.4 ($n$ = 245) waliridhika sana huku asilimia 8.8 ($n$ = 35) wakikosa kuridhika. Wanafunzi wa Kakamega waliridhika sana na mbinu zao za kijifunza kuliko wa Kisumu, japo kwa kiwango kidogo. Aidha, matokeo ya utafiti yanadhihirisha kuwa wanafunzi hawa (kijumla 539 (55.7%)) walikuwa na mielekeo chanya kuhusu mbinu walizozitumia wenyewe kujifunzia Kiswahili. Hii inaonyesha kuwa wanafunzi walifurahia na kutosheka na mbinu walizozitumia kujifunzia lugha ya Kiswahili; wengi wao walijituma kwa kujitengea muda wa kusoma na kudurusu mada zake huku wakipata maelekezi kutoka kwa walimu wao na wenzao Kakamega

Wanafunzi walikubali kuwa walisoma vitabu vya hadithi kwa asilimia 62.7 ($n$ = 356) Kakamega. Katika kaunti ya Kisumu, asilimia 58.2 ($n$ = 232) walikubali kusoma vitabu hivyo vya hadithi. Wanafunzi katika kaunti zote mbili walidokeza kuwa walisoma vitabu vya hadithi hivyo,

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1551

walionyesha mielekeo chanya kuhusu usomaji kama mbinu ya kujifunzia. Matokeo haya ni sawa na ya Babusa (2010) aliyegundua kuwa idadi kubwa ya wavulana na wasichana walionyesha mielekeo chanya kuhusu Kiswahili kwa kukubali kuwa wanafurahia kusoma riwaya, magazeti na majarida ya Kiswahili. Wanafunzi wengi waliamini kuwa mazoezi waliyopewa katika somo lenyewe yalifaa zaidi na kutosha katika kaunti ya Kakamega kwa asilimia 86.3 (*n* = 490) na kufaa kwa asilimia 74.4 (*n* = 297) Kisumu. Katika ujifunzaji wa L2; jambo la kimsingi ni kuwapa wanaojifunza mazoezi wanayoweza kufanya ndipo waweze kuimudu kikamilifu. Walimu walihakikisha kuwa wamekuza ujuzi wa wanafunzi wao katika lugha hivyo waliwapa mazoezi faafu na yaliyowaridhisha. Matokeo haya yanalingana na maoni ya Kimani (2015) aliyesisitiza kuwa mbinu ya mazoezi imejengeka kwenye msingi wa mbinu ya mawasiliano kwa kuboresha stadi za lugha (kusoma, kuandika, kusikiliza na kuzungumza) kwani ukosefu wa mazoezi mwafaka yalichangia kwenye ukosefu wa umilisi wa mazungumzo ya wanafunzi. Hata hivyo, madai haya yalikinzana na matokeo ya Wambui (2017) yaliyodhihirisha kuwa wanafunzi hawashirikishwi ipasavyo katika mazoezi yanayoweza kuimarisha umilisi wao hasa katika stadi kuu za lugha; Sarufi na mazungumzo.

Wazazi na walezi wa wanafunzi katika kaunti ya Kakamega walikadiriwa kuwa na mchango mkubwa katika maendeleo ya wanafunzi somoni kwa asilimia 80.5 (*n* = 459). Katika kaunti ya Kisumu, mchango wa wazazi na walezi ulikadiriwa kwa asilimia 78.9 (*n* = 315). Wazazi na walezi wa Kakamega walikuwa na mchango zaidi kuliko wa Kisumu kutokana na walivyoithamini somo na shughuli zao za kila siku (kukosa muda wa kufuatilia maendeleo ya wanao) kutokana na hali kuwa huenda hawakulithamini somo hili kama masomo mengine. Matokeo haya yanalingana na ya Mukhwana (2014) aliyegundua kuwa wazazi wanaitazama lugha ya Kiswahili kama kizuizi katika maendeleo ya wanao katika masuala ya kielimu; kwa wazazi wengi hasa wa mijini, lugha ya kiusomi ni Kiingereza na wala si Kiswahili.

Aidha, wanafunzi waliweza kukadiria kwa asilimia kubwa; 79.9% (wanafunzi 774) kuwa wazazi na walezi wao walihusika katika ujifunzaji wao ili kuimarisha ujuzi wao. Pia, walidokeza na kubainisha kwa asilimia 55.9 (435) kuwa waliweza kuhusika kila mara bali mara chache kwa asilimia 44.1 (343) katika ujifunzaji wao kwa jumla. Kulingana na maoni haya, wanafunzi walidhihirisha kuwa na mielekeo chanya kuhusu michango ya wazazi wao katika ujifunzaji wao. Maoni haya yalilingana na ya Owala (2014) aliyegundua kuwa wazazi waliathiri wanafunzi wao kuhusu ujifunzaji wao wa L2 kwa kuwahimiza kufurahia lugha na kufanya vyema katika lugha hiyo kwa kufuatilia matokeo yao na kuwazawadi walipofanya vyema shuleni.

Katika kaunti ya Kakamega asilimia 67.4 (*n* = 382) walikubali kuwa walishirikishwa vilivyo katika ufunzaji wao na kukataa kwa asilimia 17.3 (*n* = 98). Katika kaunti ya Kisumu, asilimia 65.9 (*n* = 263) walikubali huku asilimia 18.8 (*n* = 75) wakikataa. Kijumla asilimia 66.7 (*n* = 645) walikubali kushirikishwa vilivyo huku asilimia 17.9 (*n* = 173) wakikataa. Matokeo haya yanadhihirisha kuwa wanafunzi walikuwa na mielekeo chanya kuhusu mbinu zilizotumiwa na walimu kuwafunza Kiswahili kwa kuwa waliweza kushirikishwa vilivyo katika ujifunzaji. Katika ufunzaji na ujifunzaji mwafaka, anayejifunza anastahili kushirikishwa kikamilifu katika kila jambo linalofanywa ndipo ajifunze vyema hasa kutokana na uwezo wa kuchangia masomoni na kujigundulia mambo. Haya yanalingana na mapendekezo ya wataalamu wa kifalsafa, kisaikolojia na kielimu wanaosisitiza kuwa ufundishaji unaofaa unastahili kuhusisha zaidi matumizi ya mbinu na vifaa vya ufundishaji ambavyo humshirikisha mwanafunzi (Mlay, 2010). Maoni haya yanawiana na ya Ahmad na Aziz (2009) waliotambua kuwa wanafunzi walikadiria kuwa madarasa yao yalitawaliwa nao; matendo mengi yalielekezwa na kutekelezwa na wanafunzi wenyewe kuliko walivyotenda walimu wao bali yalikinzana na maoni ya Oloo (2018) iliyedhihirisha kuwa walimu walitawala sana shughuli ya ufunzaji na ujifunzaji wa Kiswahili madarasani mwao. Hivyo, wanafunzi wanapokosa

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1551

kushirikishwa kikamilifu katika mchakato wa kujifunza, wao huishia kufeli katika mitihani na matokeo yao duni ni ishara tosha kuwa mbinu hii inafaa kubatilishwa (wanafunzi washirikishwe) iwapo walimu wanatarajia kupata matokeo yanayoridhisha katika somo la Kiswahili.

Wanafunzi walikubali kuwa walimu wa Kiswahili waliwahimiza kutumia Kiswahili kwa asilimia 30.3 (*n* = 172) na kukataa kwa asilimia 62.5 (*n* = 354) Kakamega huku asilimia 34.1 (*n* = 136) wakikubali na asilimia 56.4 (*n* = 225) wakikataa Kisumu. Hii inadhihirisha kuwa wanafunzi walikuwa na mielekeo hasi kuhusu mbinu hii kwani walihitaji mahimizo mengi kutoka kwa walimu wao bali hawakuyapata. Mielekeo hii ilibainika sana Kakamega na mashambani hali inayoweza kuelezwa kuwa ilichangiwa na hali kuwa walimu katika maeneo haya walitawaliwa na imani yao kuhusu mielekeo ya wanafunzi wao kwa somo. Madai haya yanawiana na ya Onyango (2008) aliyebainisha kuwa mwalimu anaweza kuwapa wanafunzi wake motisha wanapojifunza L2 kwa kuwapa ushauri wa kimasomo ili kuwatia moyo. Kaunti ya Kakamega ilikuwa na wanafunzi wengi waliokubali kuwa maandalizi yao yalikuwa toshelevu kwa asilimia 64 (*n* = 363) bali asilimia 49.6 (*n* = 198) ilikubali Kisumu. Wanafunzi walidhihirisha kuwa walikuwa na mielekeo chanya kuhusu mbinu za kufunzia zilizotumika; waliamini wameandaliwa vya kutosha katika somo. Matokeo haya kuhusu maandalizi yanaweza kueleza ni kwa nini wanafunzi walifanya vyema katika mtihani wa Insha Kakamega kuliko Kisumu kwani maandalizi mwafaka huwapa imani kuu katika kufuzu kwani wao huishia kujiamini. Madai haya yanalingana na maoni ya Simiyu (2013) kuwa kukamilisha silabasi mapema hukuza dhana ya kujiamini na kuwaondolea wanafunzi hofu inayochangia na kuathiri kwa njia hasi matokeo yao.

Kitabu cha kiada kilichotumika katika ufunzaji wa Kiswahili kilikuwa Kiswahili Kitukuzwe kilichotumika sana kikaunti na kimaeneo kwa asilimia iliyokaribiana sana japo ilitumika sana Kakamega kuliko kilivyotumika Kisumu. Kijumla, kilitumika kwa asilimia 88.4 (*n* = 857). Wanafunzi walidhihirisha mielekeo chanya kuhusu matumizi ya kifaa hiki katika ufunzaji na ujifunzai wao. Hata hivyo, matumizi ya kifaa kimoja sana kina changamoto zake katika kukuza stadi za lugha miongoni mwa wanafunzi; hukosa kuimarika kikamilifu kwani lugha huimarishwa kupitia mbinu na vifaa mbalimbali vinavyovutia na kupanua fikra zaidi. Matokeo haya yanalingana na maoni ya Ogero (2012) aliyethibitisha kuwa vitabu vya kiada vilitumika kama vifaa vikuu katika ufundishaji na ujifunzaji.

**Jedwali 2: Mbinu zilizochangamkiwa zaidi**

| Mbinu | Inaridhisha | | | | Hairidhishi | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | KAKAMEGA | | KISUMU | | KAKAMEGA | | KISUMU | |
| | % | n | % | n | % | n | % | n |
| Mihadhara | 93.3 | 550 | 93.7 | 374 | 6.7 | 38 | 6.3 | 25 |
| Maonyesho | 82.2 | 467 | 74.9 | 299 | 17.8 | 101 | 25.1 | 100 |
| Majadiliano | 55.8 | 317 | 65.2 | 260 | 44.2 | 251 | 34.6 | 138 |
| Masimulizi | 96.5 | 548 | 93.2 | 372 | 3.5 | 20 | 6.8 | 27 |
| Maswali na majibu | 66.9 | 380 | 67.9 | 271 | 32.9 | 187 | 31.8 | 127 |

Mbinu iliyochangamkiwa sana Kakamega ilikuwa masimulizi (96.5%) na mihadhara (93.3%), ikifuatwa na maonyesho (82.2%) maswali na majibu (66.9%) na majadiliano (55.8%). Kisumu, mbinu ya mihadhara (93.7%) na masimulizi (93.2%) zilichangamkiwa sana zikifuatwa na maonyesho (74.9%), maswali na majibu (67.9%) kisha majadiliano kwa kiwango cha chini zaidi (65.2). Ni dhahiri kuwa mbinu zilizotumika sana (maswali na majibu pamoja na majadiliano) ndizo zilizochangamkiwa kwa viwango vya chini zaidi bali zilizotumika kwa viwango vya chini (masimulizi, mihadhara na maonyesho) ndizo zilizochangamkiwa sana na wanafunzi katika

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1551

kaunti zote mbili. Hii inabainisha kuwa mbinu zinazotumika kila mara kufunzia sizo zinazochangamkiwa na wanafunzi hivyo kuathiri ufunzaji wao na hatimaye umilisi wa lugha na matokeo yao katika somo. Hivyo basi, kuna haja ya kujumuishwa kwa mbinu hizi (mbinu mseto) wakati wa kufunza ili Kiswahili kifundishwe kwa ufasaha zaidi na wanafunzi waweze kukimudu kwa ukamilifu mkuu. Haya yanaoana na maoni ya Mukwa na Too (2014) wanaosisitiza kuwa walimu wanafaa kutumia mbinu zinazowavutia wanafunzi kwa sababu ujifunzaji hutokea hasa palipo na kiwango cha juu cha ilhamu (msukumuo na ari ya kufanya jambo) ya wanafunzi.

Isitoshe, kwa pamoja, walimu wao walitumia sana maswali na majibu; 893 (92.5%) kufunzia somo hili madarasani mwao ikifuatwa kikaribu na majadiliano 837 (86.8%) na masimulizi 697 (72.6%). Isitoshe, walimu waliweza kutumia mihadhara kwa asilimia 60.6 (579) bali mbinu ya maonyesho ilikadiriwa kwa asilimia 35.5 (342) kuwa ndiyo iliyotumiwa kwa nadra sana kuwafunzia Kiswahili. Matokeo haya yanatofautiana na mbinu ambazo wanafunzi hawa walizichangamkia; wao walichangamkia sana masimulizi (95.1%) na mihadhara (93.5%) ikifuatwa na maonyesho (79.2%), maswali na majibu (67.3%) huku majadiliano ikichangamkiwa kwa kiwango cha chini zaidi (59.7%). Hata hivyo, walimu wao walitumia sana mbinu ambazo hawakuzichangamkia walipowafunza jambo ambalo huenda liliwafanya wakose kumakinika masomoni hivyo kuathiri ujifunzaji wao na hatimaye umilisi wao wa lugha na matokeo yake katika mitihani. Hivyo basi, kuna haja ya kujumuishwa kwa mbinu hizi (mbinu mseto) wakati wa kufunza ili Kiswahili kifundishwe kwa ufasaha zaidi na wanafunzi waweze kukimudu kwa ukamilifu mkuu kulingana na maoni ya Mukwana na Too (2014).

**Jedwali 3: Maoni ya walimu na wakuu wa idara**

| Kauli | | Nakubali | | | | Sina Uhakika | | | | Nakataa | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | KK | | KSM | | KK | | KSM | | KK | | KSM | |
| Ninafunza somo langu la pili | Mw | 66.7 | 8 | 83.3 | 10 | 0 | 0 | 0 | 0 | 33.3 | 4 | 16.7 | 2 |
| | Mk | 75 | 9 | 75 | 9 | 0 | 0 | 0 | 0 | 25 | 3 | 25 | 3 |
| Walimu hutawala somo | Mw | 33.3 | 4 | 50 | 6 | 25 | 3 | 25 | 3 | 41.7 | 5 | 25 | 3 |
| Stadi za kusikiliza na kuongea husisitizwa sana | Mw | 75 | 9 | 66.7 | 8 | 25 | 3 | 8.3 | 1 | 0 | 0 | 25 | 3 |
| Vifaa vya kufunzia vinatosha | Mw | 58.3 | 7 | 66.7 | 8 | 0 | 0 | 0 | 0 | 41.7 | 5 | 33.3 | 4 |
| | Mk | 75 | 9 | 54.5 | 6 | 0 | 0 | 0 | 0 | 25 | 3 | 45.5 | 5 |
| Mbinu hizi hutumika; Kidijitali | Mw | 41.7 | 5 | 58.3 | 7 | 0 | 0 | 0 | 0 | 58.3 | 7 | 41.7 | 5 |
| | Mk | 18.2 | 2 | 33.3 | 4 | 0 | 0 | 0 | 0 | 81.8 | 9 | 66.7 | 8 |
| Mseto | Mw | 50 | 6 | 50 | 6 | 16.7 | 2 | 0 | 0 | 33.3 | 4 | 50 | 6 |
| | Mk | 33.3 | 4 | 33.3 | 4 | 0 | 0 | 0 | 0 | 66.7 | 8 | 66.7 | 8 |
| Kikoa | Mw | 58.3 | 7 | 33.3 | 4 | 0 | 0 | 0 | 0 | 41.7 | 5 | 66.7 | 8 |
| | Mk | 54.5 | 6 | 33.3 | 4 | 0 | 0 | 0 | 0 | 45.5 | 5 | 66.7 | 8 |

*Mw –Mwalimu; Mk- Mkuu wa Idara*

Matokeo ya utafiti huu kupitia majibu kwenye hojaji yalidhihirisha kuwa wengi wa walimu walifunza masomo yao ya pili; japo wale wa Kisumu walionekana kufunza sana masomo hayo wakilinganishwa na wenzao wa Kakamega. Hii inaweza ikaelezea kwa nini kiwastani wanafunzi walipata alama za chini na kufeli katika somo hili Kisumu kuliko wale wa Kakamega kwani walimu wa Kisumu walikuwa na kibarua kigumu zaidi katika maandalizi na ufunzaji wa masomo yote mawili hivyo kuathiri ujifunzaji wa wanafunzi wao. Matokeo haya yanathibitisha madai ya Oloo (2018) kuwa kazi nyingi ya mwalimu ndicho kigezo kikuu zaidi ambacho kinazuia walimu kuteua na kutumia mbinu mwafaka katika ufunzaji na ujifunzaji wa ufahamu hivyo kuathiri

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1551

mchakato huo mzima. Walimu walidai kuwa wanafanya kazi nyingi sana zisizowaruhusu kujiandaa kwa kutafuta nyenzo na kutumia mbinu bora za ufundishaji kwani walipewa vipindi vingi vya Kiswahili na masomo mengine walioyasomea kama vile Historia, Jiografia, Hisabati na hata somo la Dini.

Asilimia 33.3 ya walimu Kakamega na 50 Kisumu walikubali kuwa walitawala masomo ya Kiswahili madarasani mwao huku wakikataa kwa asilimia 41.7 Kakamega na 25 Kisumu kuonyesha kuwa wanafunzi wao waliweza kushirikishwa vilivyo masomoni. Hata hivyo, ni wazi kuwa walimu walitawala sana masomo madarasani Kisumu kuliko Kakamega. Hii inaashiria kuwa walimu walikuwa na mwelekeo hasi kuhusu kuwashirikisha wanafunzi kikamilifu masomoni; wachache tu ndio waliotumia mbinu ya ugunduzi inayowapa fursa wanafunzi kuyatawala masomo yao na kujigundulia mambo kivyao. Mbinu ya ugunduzi ndiyo inayopendekezwa na watafiti wengi wa L2 kwani kiasi kidogo sana cha sintaksia ya lugha ndicho mtu anaweza kufunzwa madhali mambo mengi sana mtu mwenyewe hujigundulia (Onyango, 2008). Matokeo haya yanaonyesha kuwa mhimili wa nadharia ya utambuzi kuhusu ushirikishi haukuzingatiwa pakubwa madhali walimu na wanafunzi hawakushirikiana vilivyo katika ufunzaji na ujifunzaji wa Kiswahili hivyo kuathiri ujifunzaji na hatimaye matokeo katika somo lenyewe. Hii inadhihirisha kuwa mbinu inayotumiwa kufunzia huweza kuathiri ujifunzaji wa wanafunzi na hatimaye kuonekana katika matokeo yao; wanafunzi wa Kakamega walioshirikishwa zaidi waliweza kufuzu vyema kimasomo. Matokeo haya yanaoana na maoni ya Chika (2012).

Hata hivyo, walimu katika kaunti ya Kisumu walitawala sana ufunzaji na ujifunzaji hali iliyochangia katika wanafunzi wao kutofuzu vyema katika somo la Kiswahili; hivyo iliathiri kwa njia hasi matokeo hayo (Tazama *Jedwali 4*). Matokeo haya yanadhhirisha kuwa mbinu isiyoshirikishi ina athari hasi katika ufunzaji, ujifunzaji na matokeo ya wanafunzi somoni madhali maarifa yanayopokelewa kupitia njia hii hayahifadhiwi kwa muda mwingi hivyo hayawezi kutumika katika mazingira mapya na wanafunzi wenyewe. Matokeo haya yanasawiana na maoni ya Mukwana na Too (2014) waliosisitiza kuwa mbinu ambazo hazimhusishi mwanafunzi si bora kwa kuwa wanafunzi huachwa nje ya mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji wa somo ambapo mwalimu ndiye huchukua usukani na kutawala.

Walimu wa Kiswahili walikadiria walivyotumia mbinu za kidijitali kufunzia mada mbalimbali za somo hilo (*Jedwali 3*). Maoni haya yanalingana na ya wanafunzi waliohusika katika utafiti huu. Matokeo haya yanadhihirisha wazi kuwa mbinu hizi hazitumiki sana kufunzia mada za Kiswahili japo kiwango cha matumizi kilionekana kuwa afadhali Kisumu kuliko hali ilivyokuwa Kakamega. Maoni haya yalionekana kulingana kiasi na kukinzana kiasi na maoni ya wanafunzi wao waliokadiria kuwa mbinu hii ilikosa kutumika sana Kakamega ikilinganishwa na hali ilivyokuwa Kisumu (Tazama *Jedwali 1*). Hata hivyo, ni bayana kuwa walimu wengi hawakuzingatia mbinu hii walipofunza mada za somo hili madarasani mwao katika kaunti zote mbili kutokana na ukosefu wa muda na vifaa vinavyohitajika kufanikisha ufunzaji wa kidijitali pamoja na kazi nyingi walizokuwa nazo walimu. Matokeo haya yanalingana na kauli iliyotolewa na Miima (2014) kuwa katika kaunti ya Kakamega walimu wachache tu ndio waliotumia vifaa vya kidijitali kufunzia lugha ya Kiswahili, wengi wao walifurahia na kuridhika kutumia mbinu za kijadi au za kawaida kufunzia. Pia, mielekeo hasi ya walimu kuhusu usetaji wa vifaa vya kidijitali katika ufunzaji huathiri kwa njia hasi matumizi ya vifaa vya kidijitali. Zaidi ya hayo, walimu hawakutumia vifaa hivyo kutokana na ukosefu wa muda na vifaa vyenyewe, ukosefu wa ujuzi mwafaka wa kuvitumia pamoja na misaada mbalimbali.

Aidha, mbinu ya kikoa ilidhihirika kutumiwa sana Kakamega kuliko ilivyozingatiwa Kisumu (*Jedwali 3*). Hii inaweza kuelezwa kuwa ilisababishwa pakubwa na idadi ndogo ya walimu wa Kiswahili katika shule za upili nchini hasa katika shule za Kakamega. Hata hivyo, maoni

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1551

haya kuhusu matumizi ya mbinu ya kikoa yalikinzana na yale ya wanafunzi wao walioamini kuwa mbinu ya kikoa ilitumika sana Kisumu (Tazama *Jedwali 1*). Huenda wanafunzi wenyewe hawakuelewa maana ya mbinu hii ndiposa maoni yao yakatofautiana na kauli za walimu wao ambao walikuwa na uelewa mkuu wa mbinu hii. Mbinu mseto iliweza kukadiriwa na walimu kwa asilimia 50 Kakamega na 50 Kisumu kuwa ilitumiwa bali asilimia 33.3 na 50 ikikataa Kakamega na Kisumu mtawalia. Mbinu hii ilionekana kuwa ilitumika kwa kiwango sawa katika kila kaunti japo asilimia 16.7 haikuwa na uhakika kuhusu matumizi yake Kakamega. Matokeo haya yanalingana kwa karibu na yale yaliyodokezwa na wanafunzi kuhusu matumizi ya mbinu hii ya kuseta mada za somo la Kiswahili (Tazama *Jedwali 1*). Udhaifu katika matumzi ya mbinu hii ilibainika wazi kuonyesha kuwa walimu wengi hawatumii mbinu hii sana wanapofunza mada za Kiswahili. Matokeo haya yanalingana na ya Odhiambo (2012) aliyesema kuwa mtaala kupitia utaratibu wa kusetwa kwa masomo ulikuwa mpana zaidi na kuwa walimu hawajapata maandalizi ya kutosha kulingana na matumizi yake; mbinu mseto. Aidha, walimu hawa walidhihirisha kuwa ilikuwa rahisi kuseta mada za Kiswahili kwa asilimia 25 Kakamega na 50 Kisumu huku asilimia 33.3 Kakamega na 25 Kisumu ikikataa bali asilimia 41.7 na 25 ikikosa uhakika Kakamega na Kisumu kitaratibu. Mada kusetwa wakati wa kufunza ilikadiriwa kuwa rahisi Kisumu kuliko ilivyochukuliwa kuwa Kakamega. Hata hivyo, ni wazi kuwa kuseta mada hizo ilikuwa tatizo kwa walimu wengi.

Walipoulizwa iwapo maandalizi ya kufunza Kiswahili ni mepesi na ya haraka, asilimia 58.3 ($n$ = 7) na 33.3 ($n$ = 4) walikubali kuwa ni mepesi, asilimia 25 ($n$ = 3) na 50 ($n$ = 6) ikikataa huku asilimia 16.7 ($n$ = 2) na 16.7 ($n$ = 2) wakikosa msimamo Kakamega na Kisumu mtawalia. Kwa pamoja, asilimia 50 ($n$ = 12) ya walimu ilidhihirisha kuwa maandalizi yanayohitajika katika ufunzaji wa Kiswahili si ya haraka wala kuwa mepesi, asilimia 37.5 ($n$ = 9) wakikubali kuwa ni haraka na mepesi huku asilimia 12.5 ($n$ = 3) wakikosa msimamo halisi. Matokeo haya yanadhihirisha kuwa maandalizi haya yalichukuliwa kuwa mepesi sana Kakamega na mashambani kuliko Kisumu na mijini. Maandalizi haya yakiwa magumu kwa walimu wengi, huenda yakawa kuwa wengi wao hukosa kujiandaa vya kutosha au hata hujiandaa kwa kiasi tu hivyo kuathiri utendakazi wao madarasani. Matokeo haya yanawiana na maoni ya Melly (2019) aliposisitiza kuwa maandalizi kabla ya kuwasilisha somo ni muhimu katika kufanikisha ubora wa somo.Madai haya yanalingana na yale ya Odhiambo (2012).

Walimu wa Kisumu walionekana kuthamini sana hali ya kutenganisha Lugha na Fasihi ya Kiswahili. Hii ni kwa kuwa asilimia 83.3 ($n$ = 10) yao ilidhihirisha manufaa makuu ya kuzitenganisha Kisumu huku asilimia 75 ($n$ = 9) ikiunga mkono maoni haya Kakamega. Aidha, asilimia sawia ya 16.7 ($n$ = 2) ikikadiria manufaa ya wastani bali asilimia 8.3 ($n$ = 1) ikidhihirisha kuwa ina mchango mdogo sana. Kutenganisha Lugha na Fasihi ilikadiriwa kuwa na manufaa sana miongoni mwa walimu wa Kisumu kushinda wa Kakamega. Hii ilidhihirisha wazi kuwa walimu walitamani Lugha na Fasihi zitenganishwa kama masomo mawili tofauti. Matokeo haya yanawiana na mapendekezo yaliyotolewa na Tume ya Koech (1999) kuwa masomo ya Lugha ya Kiswahili na Fasihi ya Kiswahili yafundishwe kama masomo mawili tofauti. Ingawaje, walimu waliweza kuziseta mada za somo na kufurahia jambo hili Kakamega kuliko Kisumu. Matokeo haya yanaonyesha kuwa walimu wengi walipendelea masomo haya yatenganishwe; yasifunzwe kwa pamoja hivyo kudokeza mielekeo hasi kuhusu mbinu mseto na ufunzaji wa Lugha na Fasihi ya Kiswahili kama somo moja. Matokeo haya yanaonyesha kuwa walimu wanapitia changamoto mada hizi zinapojumuishwa tukawa na somo moja la Kiswahili. Maoni haya yanalingana na ya Akaka (2017) aliyebaini kuwa uamuzi wa kuunganisha vipengele hivi viwili vya Kiswahili (Lugha na Fasihi) umekuwa changamoto kwa walimu madhali wao hujikuta wakiegemea zaidi upande wa Fasihi kuliko Lugha. Mintarafu ya kuwa mwalimu mmoja hawezi kumudu nyanja zote za

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1551

somo la Kiswahili baadhi yao hukwepa kufunza lugha kwa hofu ya kuulizwa maswali kuhusu mambo wasiyoyaelewa.

**Maoni ya Mudir au Mkuu wa Idara**

Kuhusu matumizi ya mbinu za kidijitali kufunzia Kiswahili, asilimia 18.2 na 33.3 yao walikubali bali asilimia 81.8 na 66.7 wakikataa katika kaunti za Kakamega na Kisumu mtawalia. Matokeo haya ya majibu ya maswali ya mahojiano yanadhihirisha wazi kuwa mbinu hizi hazitumiki sana kufunzia mada za Kiswahili japo kiwango cha matumizi kilionekana kuwa afadhali Kisumu kuliko hali ilivyokuwa Kakamega. Maoni haya yalilingana na yaliyodokezwa na walimu kuhusu matumizi ya mbinu hii ya kiteknolojia (*Jedwali 3*). Aidha, ilibainika wazi kuwa vifaa vya kidijitali havikutumiwa kufunzia Kiswahili kwani walimu waliohusika walikadiria kutotumika kwa santuri, tepurekoda, kanda na video kwa asilimia 79.2 ($n$ = 19), 79.2 ($n$ = 19), 75 ($n$ = 18) na 37.5 ($n$ = 9) mtawalia. Vifaa hivyo vilikadiriwa kutumika mara moja moja kwa asilimia 20.8 ($n$ = 5), 20.8 ($n$ = 5), 20.8 ($n$ = 5) na 54.3 ($n$ = 13) mtawalia. Matokeo haya yanaashiria kuwa walimu wengi hawakutumia mbinu za kidijitali kufanikisha ufunzaji na ujifunzaji wa Kiswahili katika shule za upili katika kaunti husika Matokeo haya yanalingana na maoni ya Kimani (2015) kuwa walimu wengi hutumia mbinu za kitambo na vifaa kongwe kufunzia huku wakipuuza mbinu za kisasa za kidijitali. Mbinu ya kikoa iliweza kukadiriwa kuwa ilitumika kufunzia Kiswahili kwa asilimia 54.5 Kakamega na 33.3 Kisumu huku asilimia 45.5 Kakamega na 66.7 Kisumu ikibainisha kuwa haikutumika. Hii inadhihirisha kuwa mbinu hii ilitumika sana Kakamega kuliko Kisumu. Hii inaweza kuwa imesababishwa na idadi ya walimu na idadi ya vipindi wanavyovifunza katika wiki. Wanafunzi waliofunzwa kwa mtindo huu walionekana kuwa na umilisi wa kiwango cha juu kuliko wale ambao hawakuelekezwa kikamilifu kupitia mtindo huu kutokana na uhaba wa walimu (Tazama *Jedwali 3*).

Asilimia 33.3 na 33.3 yao katika kaunti za Kakamega na Kisumu mtawalia walikubali kuwa walitumia mbinu mseto kufunzia somo la Kiswahili madarasani mwao. Hata hivyo, asilimia 66.7 na 66.7 yao ikikataa; kumaaainisha kuwa hawakuitumia kufunzia katika kaunti za Kakamega na Kisumu kimfuatano. Ni wazi kuwa mbinu hii haikutumika sana katika ufunzaji na ujifunzaji wa mada za Kiswahili hasa katika kaunti zote. Inawezekana kuwa hali hii ilichangiwa sana na ujuzi walio nao walimu katika usetaji wa mada za somo la Kiswahili. Madai haya yanawiana na maoni ya Odhiambo (2012) kama yalivyodokezwa hapo juu.

Walimu hawa waliulizwa kukadiria jinsi walivyotumia mbinu mbalimbali za kufunza na kujifunzia Kiswahili nao wakabainisha kuwa maonyesho yalitumiwa mara moja moja kwa asilimia 70.8 ($n$ = 17), kila mara kwa asilimia 4.2 ($n$ = 1) na kutotumika kwa asilimia 25 ($n$ = 6). Maswali na majibu yalitumiwa kila mara kwa asilimia 79.2 ($n$ = 19), mara chache kwa asilimia 12.5 ($n$ = 3) bali hayakutumika kwa asilimia 8.3 ($n$ = 2). Majadiliano yalikadiriwa kutumiwa kila mara kwa asilimia 70.8 ($n$ = 17), mara chache kwa asilimia 29.2 ($n$ = 7) lakini mihadhara iliweza kukadiriwa kuwa ilitumiwa mara moja moja kwa asilimia 70.8 ($n$ = 17), kila mara kwa asilimia 25 ($n$ = 6) huku ikikosa kutumika kwa asilimia 4.2 ($n$ = 1). Maoni haya yalilingana na yaliyotolewa na wanafunzi kuwa mbinu iliyozingatiwa zaidi ilikuwa maswali na majibu ikifuatwa na majadiliano huku mihadhara na maonyesho ikibainika kutumika kwa nadra sana (Tazama *Jedwali 1*). Hata hivyo, ni dhahiri kuwa mbinu zilizotumika sana (maswali na majibu pamoja na majadiliano) ndizo zilizochangamkiwa kwa viwango vya chini zaidi bali zilizotumika kwa viwango vya chini (masimulizi, mihadhara na maonyesho) ndizo zilizochangamkiwa sana na wanafunzi katika kaunti zote mbili (Tazama *Jedwali 2*). Hii inabainisha kuwa mbinu zinazotumika kila mara kufunzia sizo zinazochangamkiwa na wanafunzi hivyo kuathiri ufunzaji wao na hatimaye umilisi wa lugha na matokeo yao katika somo. Hivyo basi, kuna haja ya kujumuishwa kwa mbinu hizi (mbinu mseto)

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1551

wakati wa kufunza ili Kiswahili kifundishwe kwa ufasaha zaidi na wanafunzi waweze kukimudu kwa ukamilifu mkuu. Madai haya yanaoana kabisa na maoni ya Oloo (2018) aliyetambua kuwa wanafunzi walipendelea mbinu ambazo walimu hawakuzitumia kila wakati walipofunza na kusoma Ufahamu nao; mathalani njia ya kidrama, kusimulia hadithi na mjadala. Hivyo basi, kuna haja ya kujumuishwa kwa mbinu hizi zinazopendelewa na wanafunzi ili ufahamu ufundishwe kwa ufasaha zaidi licha ya kutopendwa na walimu wengi.

Mbinu ya mihadhara ilitumika sana Kakamega kuliko Kisumu. Pia, ilitumika kwa mara chache kwa asilimia 66.7 ($n$ = 8) na 75 ($n$ = 9) Kakamega na Kisumu kimfuatano huku asilimia 8.1 ($n$ = 1) ikikosa kuitumia Kisumu. Matumizi ya mihadhara kwa wingi Kakamega huenda ilisababishwa na hali kuwa wanafunzi walikuwa wengi mno madarasani mwao hivyo kuwa tatizo kuu kwa walimu kuwashirikisha sana wanafunzi katika ujifunzaji wao. Pia, hali hii huenda ndiyo iliyochangia katika kuwepo kwa matokeo mabaya ya wanafunzi hawa katika somo la Kiswahili hata ingawa waliibuka washindi; kuwa kidedea kwa wenzao wa Kisumu (Tazama *Jedwali 4*). Matokeo haya yalisawiana na maoni ya Wambui (2017) kuwa walimu wengi walitumia mbinu ya mhadhara katika kufundisha sarufi huku mbinu za kisasa ambazo zinawashirikisha wanafunzi zaidi zikipuuzwa. Majadiliano yalizingatiwa kwa kina zaidi Kakamega kuliko yalivyozingatiwa Kisumu. Hii ni kutokana na ukadiriaji uliofanywa na walimu waliohusika; yalitumika kila mara kwa asilimia 75 ($n$ = 9) na 66.7 ($n$ = 8) na kutumika mara moja moja kwa asilimia 25 ($n$ = 3) na 33.3 ($n$ = 4) Kakamega na Kisumu kitaratibu. Madai haya ni sawa na matokeo yaliyodhihirika katika uchunguzi wa madarasa uliobainisha kuwa mijadala na mihadhara ndizo mbinu zilizotumika sana kufunzia katika shule za Kakamega. Hali hii inaweza kueleza kwa nini wanafunzi wa Kakamega waliweza kufanya vyema kiasi katika mtihani wa Insha ya kiubunifu wakilinganishwa na wenzao wa Kisumu. Madai haya yanaoana na maoni ya Kang'ahi na wenzake (2012) aliyefafanua kuwa matokeo mema huhusishwa na mbinu za kufunzia zilizowapa wanafunzi fursa ya kushiriki kikamilifu katika ujifunzaji wao huku matokeo duni yakishuhudiwa katika madarasa yaliyotawaliwa na walimu katika mchakato wa kufunza na kujifunza. Kulingana naye, ni wazi kuwa mbinu za ufunzaji zina athari kubwa katika kuelekeza matokeo ya wanafunzi katika lugha ya Kiswahili.

Walimu waligawana mada katika idara na kuzifunza kwa pamoja; mbinu ya kikoa ilizingatiwa kwa viwango sawa. Walimu walikubali kuwa walitumia mbinu ya kikoa kwa asilimia sawia ya 58.3 ($n$ = 7) huku asilimia 41.7 ($n$ = 5) ikibainisha kuwa mbinu hiyo haikutumika; kila mwalimu hufunza sehemu zote peke yake katika madarasa yake. Hata hivyo, mbinu hii ilitumika sana Kakamega kuliko ilivyozingatiwa Kisumu. Mbinu hii ilikuwa na mchango wake katika ujifunzaji wa wanafunzi na hatimaye matokeo yao halimad waliweza kufidiana na kusaidiana mahali ambapo huenda mmoja alikuwa na tatizo kwalo hivyo kuwanufaisha wanafunzi wao hata zaidi na kuimarisha ujifunzaji wao. Walimu hawa walionekana kuwa na uelewa mkuu wa methali hizi; Umoja ni nguvu utengano ni udhaifu, Kidole kimoja hakivunji chawa na Jifya moja haliinjiki chungu. Matokeo haya yanalingana na maoni ya Oxford (1997) kuwa ushirikiano unafaa katika ufunzaji wa L2 maadamu inaweza kutumika katika viwango vyote vya elimu kuimarisha mawasiliano na utatuzi wa mtafaruku unaoweza kutokea kufuatia maoni tofauti.

Maoni haya yaliungwa mkono na Wakuu wa Idara waliodokeza kuwa walimu wa Kiswahili waliofunza katika shule za Kakamega walionekana kushirikiana sana katika ufunzaji wao kama walimu kwa asilimia 100 ($n$ = 12) bali wa Kisumu walionyesha kushirikiana kwa asilimia 72.7 ($n$ = 8) huku asilimia 27.3 ($n$ = 3) ikisema hawashirikiani. Ni dhahiri kuwa walimu walishirikiana katika ufunzaji katika kaunti zote ila kiwango cha kushirikiana kilionekana kuwa juu Kakamega kushinda kilivyokuwa Kisumu. Kushirikiana kunaweza kuelezea kwa nini wanafunzi walifanya vyema kiasi Kakamega

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1551

kushinda matokeo ya wanafunzi wa Kisumu. Pia, kushirikiana kuliwezekana kutokana na hali kuwa Kakamega ilionekana kuwa na upungufu wa walimu waliohitimu na wanafunzi kuwa wengi mno kuliko hali ilivyokuwa Kisumu hivyo huenda ikafafanuliwa kuwa kushirikiana kufunza kunatokana na uelewa wao kuwa mbinu hiyo ina manufaa mengi mno katika ufunzaji na ujifunzaji wa Kiswahili. Madai haya yalilingana na maoni ya Kimani (2015) aliyebainisha kuwa ushirikiano ni mbinu ya kisasa yenye matokeo mazuri.

**Mbinu za Ziada**

Kando na vitabu viteule vya Kiswahili vilivyofunzwa, wanafunzi waliweza kuvipitia vingine na walimu wao. Katika kaunti ya Kakamega asilimia 66.7 (*n* = 8) ya walimu walikubali kutumia vitabu vya hadithi huku asilimia 41.7 (*n* = 5) ikiwa na maoni hayo Kisumu. Ni dhahiri kuwa vitabu vya hadithi vilizingatiwa sana Kakamega kuliko hali ilivyokuwa Kisumu. Matumizi ya vitabu vya hadithi huenda ikawa ni mojawapo za sababu zilizowawezesha wanafunzi kufanya vyema kiasi katika shule za Kakamega na mijini kuliko wenzao wa Kisumu na mashambani. Matokeo haya yanaoana na maoni ya Chacha (2016) na Ngugi (2009) waliogundua kuwa ni dhahiri kuwa wanafunzi ambao hawasomi vitabu vya hadithi vya kutosha hawawezi kuimudu lugha kwa ufasaha. Kwa maandalizi mema zaidi na kuimarisha ujuzi wao, walimu waliwapa maswali na mitihani mingi ya Kiswahili kwa asilimia 91.7 (*n* = 11) na 83.3 (*n* = 10) Kakamega na Kisumu mtawalia. Ni wazi kuwa walimu wengi walithamini sana matumizi ya maswali na mitihani kadhaa ya Kiswahili kama njia mwafaka ya kunoa makali ya wanafunzi wao katika somo lenyewe. Hii inaonyesha kuwa maswali na mitihani mingi ya Kiswahili ilithaminiwa, japo iliangaziwa sana Kakamega kushinda Kisumu. Ni wazi kuwa mikakati hii iliyozingatiwa iliweza kuwanufaisha walimu na wanafunzi wao somoni madhali ilizaa matunda katika matokeo ya wanafunzi wao hasa katika insha ya kiubunifu (Tazama *Jedwali 4*). Maoni haya yanawiana na ya Rosenthal na Jacobson (1968) kuwa walimu walipotarajia mema kutoka kwa baadhi ya wanafunzi, walijikakamua kuhakikisha kuwa nao kama walimu waliwajibika kiutendaji huku wakitarajia makuu kutoka kwa wanafunzi wao kwa kuwapa mitihani na mazoezi mengi.

**Jedwali 4: Matokeo ya Wanafunzi katika Insha ya Ubunifu**

| Vigeu | Viwango | Mean/ Wastani | (Standard Deviation) kupotoka kwa kawaida | Alama ya chini | Alama ya juu |
|---|---|---|---|---|---|
| Kaunti | Kakamega | 49.12 | 16.14 | 16 | 88 |
| | Kisumu | 44.00 | 12.82 | 4 | 84 |
| Eneo la shule | Mashambani | 42.66 | 13.97 | 4 | 80 |
| | Mijini | 50.83 | 14.98 | 12 | 88 |
| Jinsia | Wavulana | 48.27 | 13.88 | 12 | 88 |
| | Wasichana | 45.94 | 15.95 | 4 | 88 |
| Ufaafu na utoshelevu wa mazoezi | Unafaa zaidi | 47.35 | 14.84 | 4 | 88 |
| | Unafaa kiasi | 45.95 | 15.59 | 12 | 88 |
| | Haufai kamwe | 43.41 | 16.89 | 16 | 76 |

Isitoshe, gazeti la Taifa Leo lilitumiwa sana na walimu kukuza ujuzi wa wanafunzi wao katika lugha ya Kiswahili katika kaunti ya Kakamega kuliko Kisumu. Asilimia 66.7 (*n* = 8) na 50 (*n* = 6) ilitumia gazeti hilo kufunzia mada za Isimujamii, usomaji mpana ili kufahamu masuala ibuka katika jamii, mtiririko wa mawazo katika insha ya masimulizi, tahariri, barua kwa mhariri na taarifa huku asilimia 33.3 (*n* = 4) na 50 (*n* = 6) ikikosa kutumia kifaa hiki kabisa katika Kaunti za Kakamega na Kisumu mtawalia. Ni dhahiri kuwa walimu walikuwa na mielekeo chanya kuhusu matumizi ya magazeti ya Kiswahili japo mielekeo hiyo ilitawala sana Kakamega kuliko Kisumu. Matumizi ya gazeti yalizingatiwa sana Kakamega kushinda hali ilivyokuwa Kisumu hali iliyoweza kuelezea kwa nini matokeo ya wanafunzi yalikuwa afadhali Kakamega (Rejelea *Jedwali 4*).


This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1551

Matokeo haya yanalingana na mapendekezo yaliyotolea na Owala (2014) kuwa mwalimu anayejifunza L2 afanye mipangilio ili wanafunzi waweze kununuliwa magazeti yanayohusu lugha hiyo.

Vitabu vya marudio na marejeleo mbalimbali (vitabu vya ziada) vilitumiwa na walimu ili kuendeleza ujuzi ambao tayari ulikuwa umezingatiwa madarasani. Katika kaunti ya Kisumu asilimia 91.7 (*n* = 11) ilikadiria matumizi ya vitabu vya marudio bali asilimia 8.3 (*n* = 1) ikibainika kuwa hawakutumia vitabu hivyo lakini katika kaunti ya Kakamega asilimia 100 (*n* = 12) ilikadiria matumizi haya kikamilifu. Walimu walikuwa na mielekeo chanya zaidi kuhusu matumizi ya nyenzo mbalimbali katika ufunzaji wa somo katika kaunti ya Kakamega. Matumizi ya vitabu hivi vilichangia katika kukuza na kuimarisha stadi za lugha miongoni mwa wanafunzi hivyo kuathiri matokeo yao somoni. Madai haya yanawiana na matokeo ya Batibo (2005) alipoeleza kuwa ufunzaji na ujifunzaji wa somo la Kiingereza hudorora kutokana na hali kuwa kuna uhaba na ukosefu wa vitabu vya kiada, vya marejeleo na vya ziada pamoja na ukosefu wa athari kuu ya lugha kimatumizi kwa kukosa kutambua umuhimu wa lugha yenyewe.

**Chati 1: Maoni ya walimu kuhusu vigezo vilivyoathiri ufunzaji**




This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1551

Kuna baadhi ya mambo ambayo yaliathiri uteuzi wa mbinu zilizotumiwa na walimu kufunza mada mbalimbali za Kiswahili. Walimu walihitajika kutambulisha baadhi ya mambo yaliyoathiri ufunzaji wao kwa kukubali au kukataa kuhusu masuala mbalimbali. Kutokana na maoni yao, ni wazi kuwa mielekeo ya wanafunzi iliathiri kwa njia sawa (91.7%) ufunzaji wa Kiswahili katika kaunti zote, Kisumu ilitawala katika vigezo vyote isipokuwa mielekeo ya walimu; iliyoongoza Kakamega kwa asilimia 50. Matokeo haya yanalingana na maoni ya Akaka (2017) aliyebainisha kuwa walimu wanaofunza lugha hutumia zaidi ya mbinu moja ya ufunzaji kutegemea malengo ya somo, sifa za wanafunzi na kadhalika. Hivyo basi, mwalimu wa Kiswahili anapaswa kufahamu mbinu na mikakati kadha wa kadha ya ufunzaji wa lugha ya Kiswahili ili aweze kutambua mbinu ambazo zinafaa kutumiwa kufundishia kutegemea tofauti za wanafunzi darasani.

Walimu walikubali kuwa idadi ya vipindi walivyovifunza katika wiki iliathiri uteuzi huo kwa asilimia 83.3 ($n$ = 10) na 66.7 ($n$ = 8) Kisumu na Kakamega. Hii inaonyesha kuwa walimu wa Kisumu waliamini kuwa vipindi hivyo vilikuwa na mchango mkuu katika uteuzi wao kuliko wenzao wa Kakamega. Hali hii huenda ilisababishwa na uzoefu wao wa kufunza masomo yao mawili; Kiswahili na somo la pili walilisomea na kuhitimu kwalo chuoni. Maoni haya yanawiana na ya Oloo (2018) kuwa kazi nyingi ya mwalimu huathiri uteuzi na matumizi ya mbinu mwafaka katika ufunzaji na ujifunzaji hivyo kuathiri mchakato huo mzima.

Pia, idadi ya wanafunzi katika kila darasa na viwango vyao viliathiri uteuzi wa mbinu za kufunzia (Rejelea *Chati 1*). Walimu katika kaunti ya Kisumu waliamini sana kuwa idadi ya wanafunzi darsani na viwango vyao viliathiri ufunzaji wakilinganishwa na wale wa Kakamega. Matokeo haya yanaoana na ya Oloo (2018) aliyegundua kuwa idadi kubwa ya wanafunzi madarasani iliathiri ufunzaji kwani iliwazuia walimu kuteua na kutumia mbinu mwafaka katika ufunzaji na ujifunzaji wa Ufahamu. Pia, yanalingana na ya Mlay (2010) aliyebainisha kuwa mambo mengine kama madarasa yaliyojaa kupita idadi kamili, idadi isiyolingana ya walimu kwa wanafunzi pamoja na ukosefu wa vifaa vya kimsingi kama vile viti huathiri mchakato wa ufunzaji na ujifunzaji. Aidha, walimu wengi walitambua manufaa ya kutumia mbinu shirikishi kufunzia ila idadi ya wanafunzi madarasani mwao na idadi ya vipindi vinavyofunzwa nao katika wiki ni baadhi ya mambo yaliyositisha juhudi zao za kutumia mbinu hizo kufunzia.

Isitoshe, mielekeo ya wanafunzi ilikadiriwa kuwa inaathiri ufunzaji kwa asilimia 66.6 ($n$ = 8) na 58.4 ($n$ = 7) katika kaunti za Kisumu na Kakamega mtawalia. Walimu wa Kisumu waliamini kuwa mielekeo ya wanafunzi wao iliathiri ufunzaji wao kuliko wenzao wa Kakamega. Mielekeo hii iliathiri uteuzi wa mbinu za kufunzia hivyo kuathiri ujifunzaji na matokeo ya wanafunzi somoni. Matokeo haya yanalingana na madai ya Oloo (2018) kuwa mielekeo ya wanafunzi iliathiri uteuzi na matumizi ya mbinu za ufunzaji na ujifunzaji madhali iliwazuia walimu kuteua na kutumia mbinu mwafaka katika ufundishaji na ujifunzaji wa ufahamu.

Hata hivyo, mielekeo ya walimu ilikadiriwa kuwa na athari kiasi. Walimu katika kaunti ya Kakamega waliamini kuwa mielekeo yao ilikuwa na athari kuliko wale wa Kisumu. Matokeo haya yanaoana na yale ya Rosenthal na Jacobson (1968) waliogundua kuwa walimu wakuu na walimu wanapotarajia matokeo mabaya kutoka kwa wanafunzi wao, matokeo bila shaka huwa duni. Isitoshe, ilibainika wazi kuwa walimu walipotarajia mema kutoka kwa baadhi ya wanafunzi, walijikakamua kuhakikisha kuwa nao kama walimu waliwajibika kiutendaji huku wakitarajia makuu kutoka kwa wanafunzi wao. Hii huelezea kwa nini baadhi ya shule na wanafunzi hufanya vyema katika mitihani kwani walimu wao hutarajia makuu zaidi kutoka kwao na hufahamu namna ya kuwaelezea hayo hivyo, wanafunzi hawayachukulii kama adhabu kuu inayotolewa kwao na walimu hawa. Haya yanaonyesha wazi kuwa mielekeo yetu kuhusu

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1551

kitu, mtu, hali au jambo huwa na athari kuu katika utendaji na hatimaye matokeo yao.

Muda uliopo wa kufunzia mada za Kiswahili pia uliathiri uteuzi wa mbinu za kufunzia. Walimu wa Kisumu waliamini sana kuwa muda uliopo uliathiri ufunzaji wao wakilinganishwa na wa Kakamega. Maoni haya yanalingana na maoni ya Oloo (2018) aliyebainisha kuwa, asilimia 72 ya walimu waliamini kuwa vipindi vichache vya kusoma viliathiri uteuzi na matumizi ya mbinu mwafaka katika ufunzaji na ujifunzaji wa Ufahamu. Vilevile, yanaoana na maoni ya Wambui (2017) alyedhihirisha kuwa baadhi ya walimu walidai kuwa hawakuweza kushirikisha mbinu tofauti hasa vifaa vya kidijitali kwa sababu walikumbwa na changamoto kama vile vipindi vichache vilivyotengewa somo la Kiswahili, silibasi pana, na wanafunzi wengi madarasani mwao.

Uchunguzi uliofanywa ulibainisha kuwa walimu wa Kiswahili katika kaunti ya Kakamega walifuatilia kikaribu maendeleo ya wanafunzi wao katika somo kwa kuhifadhi vyema alama zao kushinda wa Kisumu. Walimu hawa walikuwa na alama za wanafunzi wao katika somo la Kiswahili walipofanya mtihani wa kuhitimu masomo ya shule ya msingi; KCPE kama alama za kiingilio, alama walizopata kuanzia kidato cha kwanza katika kila mjarabu na mtihani kuonyesha walivyopiga hatua somoni na alama za Kiswahili za kuhitimu masomo ya sekondari (KCSE). Hatua hii iliyochukuliwa na walimu huenda ndiyo iliyowawezesha kupata alama bora zaidi kutokana na hali kuwa walimu wao walimakinika sana katika utendakazi wao masomoni hivyo kuwapa msukumo wa kujituma na kujukumika hata zaidi. Maoni haya yanakaribiana na yaliyobainishwa na Rosenthal na Jacobson (1968) kuwa walimu na walimu wakuu wanapotarajia matokeo mabaya kutoka kwa wanafunzi wao, matokeo bila shaka huwa duni. Vilevile, ilibainika wazi kuwa walimu walipotarajia mema kutoka kwa baadhi ya wanafunzi, walijikakamua kuhakikisha kuwa nao kama walimu waliwajibika kiutendaji huku wakitarajia makuu kutoka kwa wanafunzi wao. Haya yanaonyesha wazi kuwa mielekeo yetu kuhusu kitu, mtu, hali au jambo huwa na athari kuu katika utendaji na hatimaye matokeo yetu.

## MUHTASARI NA MAPENDEKEZO

Somo hili ni muhimu sana katika ukuzaji wa maarifa na kuendeleza mawasiliano miongoni mwa watu wa taifa na mataifa mbalimbali. Mbimu za kufunza na kujifunzia somo hili zinafaa kukuzwa ili ziwe zinazowashirikisha wanafunzi zaidi na kuwachangamsha kwa kuteka makini yao vyema huku walimu wakiwa waelekezi wao. Ingawa changamoto zipo katika ufunzaji na ujifunzaji wake ni vyema kuboresha mbinu za ufunzaji wake huku nyenzo faafu hasa zinazovutia, huteka makini na kuimarisha uelewaji pamoja na kuwawezesha kukumbuka yaliyofunzwa vizuri zizingatiwe zaidi. Mielekeo hasi inayotawala miongoni mwa walimu, wanafunzi na wazazi au walezi kuhusu somo au hata mbinu za kufunza na kujifunzia somo hili iondolewe kabisa huku motisha na ushauri ukitolewa kwao kila mara kufafanua umuhimu wa kuithamini somo lenyewe.Walimu washirikishwe katika warsha na makongamano ya Kiswahili mara kwa mara ili kupiga msasa ujuzi wao ili kutosheleza mahitaji ya kijamii kitaaluma na kupata suluhu kwa baadhi ya changamoto wanazopitia katika ufunzaji wa somo lenyewe.Muda uliotengewa somo uongezwe ili walimu waweze kuwashirikisha wanafunzi katika ufunzaji shirikishi zaidi huku mbinu mseto ukizingatiwa zaidi kwa kuzingatia viwango vyake vyote sita.

Kwa sababu utafiti huu uliwahusisha wanafunzi wa kidato cha tatu pekee katika baadhi ya shule za upili katika majimbo ya Kisumu na Kakamega ipo haja ya utafiti mwingine kufanywa katika maeneo mengine na shule kadhaa za upili na msingi nchini na pia katika madarasa na vidato vingine.

## MAREJELEO

Adeyemo, S.A. (2011). The Effect of Teachers' Perception and Students' Perception of Physics Classroom Learning Environment on their Academic Achievement in Senior Secondary Schools Physics. *International*

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1551

*Journal of Educational Research and Technology*. *Vol.2, Issue 1, 2011: 74-81. ISSN 0976 -4089 Journal's URL: www.soeagra.com/ijert.htm.*

Ahmad, F. na Aziz, J. (2009). Students' Perceptions of the Teachers' Teaching of Literature Communicating and Understanding Through the Eyes of the Audience. *European Journal of social sciences, 7 (3)*, 17.

Akaka, L. (2017). Changamoto Zinazowakabili Walimu katika Ufundishaji wa Kiswahili katika Shule za Upili Nchini Kenya. *Kioo cha Lugha*, *11*(1).

Aziz, M. (2003). Organizational Role Stress among Indian Information Technology Professionals. *Asian-Pacific Newsletter on Occupational Health and Safety, 10, 31-39. Scientific Research: An Academic Publisher*.

Babusa, H. O. (2010). *Uchanganuzi linganuzi wa mielekeo na umilisi wa lugha ya Kiswahili wa wanafunzi katika mikoa ya Pwani na Nairobi nchini Kenya*.(Doctoral dissertation, Kenyatta University).

Batibo, H. (2005). *Language decline and death in Africa: Causes, consequences, and challenges* (Vol. 132). Multilingual Matters.

Cannon, C.M. na Palmiter, R.D. (2003). Reward without Dopamine. *The Journal of Neuroscience: The official Journal of the Society for Neuroscience 23 (34:10827-31*.

Chacha, S. (2016). Uhusiano wa Mikakati ya Ufundishaji wa Fasihi ya Watoto ya Kiswahili na Umilisi wa Kusoma Katika Shule za Msingi, Kasarani, Kaunti ya Nairobi, Kenya: *Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Kenyatta.(Haijachapishwa).*

Chika, P. O. (2012). The Extent of Students' Responses in the Classroom. *International Journal of Academic Research in Business and Social Sciences, 2 (1).* www.hrmars.com/journals on 02/10/2015.

Creswell, J. W. (2014). *Research Design :Qualitative, Quantitative and Mixed Methods Approaches* (4th ed). London: Sage Publications.

Cummin, G. na Lindsey, D. J. (2004). *The Relationship between Teachers literary beliefs and their instructional practices.*Educational Journal of Teaching and Learning in Diverse Settings. 1 (2), 175-188.

Ellis, R. (I997). *Instructed Second Language Acquisition*. Oxford: Basil Blackwell Ltd.

Gathumbi, A. W., & Masembe, S. C. (2005). *Principles and techniques in language teaching: A text for teacher educators, teachers, and pre-service teachers*. Jomo Kenyatta Foundation.

Guha, S. (2003). Are we all, technically prepared? Teachers' perspective on the course of comfort or discomfort in using computers at elementary grade teaching. *Information Technology in childhood Annual*, 317-349.

Henson, K. T. (2004). *Constructivist methods for teaching in diverse middle-level classrooms*. Boston, MA: Allyn & Bacon.

Hou, C. S. (2007). A study on the relationship between teacher-student style match or mismatch and English learning achievements. *Unpublished master's thesis). National Yunlin University of Science & Technology, Yunlin, Taiwan*.

Kang'ahi, M., Indoshi, F. C., Okwach, T. O., & Osodo, J. (2012). Teaching styles and learners' achievement in Kiswahili language in secondary schools. International Journal of Academic Research in Progressive Education and Development, 1(3). www.hrmars.com/journals on 02/10/2015.

KIE (2002). *Secondary Education Syllabus,* Volume one, Nairobi: K.I.E.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1551

Kimani J. N.(2015). Uhusiano wa mbinu za kufundisha sarufi na umilisi wa mazungumzo ya wanafunzi wa sekondari, Kaunti ndogo ya Thika Magharibi, Kenya.*Tasnifu ya Shahada ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Kenyatta, Kitivo cha Elimu (Haijachapishwa).*

Lighbown, P. na Spada. *(1990). Focus on Form and Corrective Feedback in Communicative Language Teaching: Effects on Second Language Learning.* Cambridge: Cambridge University Press.

Look, D. (2005). Discussion Paper: Impact of Technology on Education, PUSD Excellence committee. http://pleasanton.k12.ca.us/ Superintendent/ Downloads/Technology.pd

Magare, D. Y. (2017). Matumizi ya Majadiliano ya Vikundi katika Kufunzia Stadi za Kuzungumza katika Shule za Upili katika Tarafa ya Mososcho, Kaunti ya Kisii, Kenya. *Tasnifu ya uzamili, Chuo Kikuu cha Kenyatta, Kitivo cha Elimu (Haijachapishwa).*

Melly, K. J. (2019). Matumizi ya vifaa vya kisasa katika ufundishaji na ujifunzaji wa Sarufi:Mfano wa Shule za Upili Kaunti ndogo ya Moiben, Kenya**.** *Tasnifu ya uzamili, Chuo Kikuu cha Kibabii (Haijachapishwa).*

Miima, F. A. (2014). Integration of information communication technologies in teaching and learning of Kiswahili language in public secondary schools in Kakamega County, Kenya. *Unpublished PhD Thesis, Kenyatta University*.

Mlay, N. (2010). *The influence of the language of instruction on students' academic performance in secondary schools: A comparative study of urban and rural schools in Arusha-Tanzania* (Master's thesis, University of Oslo).

MOE (2005). *KESSP 2005-2010*. Nairobi: Ministry of Education.

Mukhwana, A.(2014). Attitude towards Kiswahili in urban Kenya. *International Journal of Scientific Research and Innovative Technology, 1(3).*

Mukwana, C.W. & Too, J. (2014). *General Instructional Methods.* Moi University Press. Eldoret.

Nakhumicha, S. M. (2013). Factors Affecting Academic performance in Secondary Schools in Kenya. A case of Trans-Nzoia West District.d*MPHL Thesis). Moi University, Eldoret, Kenya*.

Ngugi wa Thiongo (2009). *Remembering Africa.* East African Educational Publishers. Nairobi, Kenya.

Odhiambo, (2012). *Taskforce on the Realignment of the Education Sector to the Constitution of Kenya 2010: Towards a Globally Competitive Quality Education for Sustainable Development.* Report of the Task Force-MOE, Kenya.

Ogero, J. O. (2012). Institution based factors influencing students' performance in Kiswahili at KCSE in public schools in Sameta Division Kisii County Kenya. *Unpublished MED Thesis, Kenyatta*.

Oloo, M. A. (2018). Masuala yanayoathiri Ufunzaji na Ujifunzaji wa somo la Ufahamu katika shule za upili katika kaunti ya Kisumu nchini Kenya. *Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia cha Masinde Muliro (MMUST). (Haijachapishwa).*

Onyango, J. (2008). *Second Language Learning.* Unpublished module, Kenyatta University.

Opunde, S. (Haijulikani). Mwelekeo Mseto katika Ufundishaji wa Lugha ya Kiswahili. *Karatasi ya utafiti, Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia cha Masinde Muliro (MMUST).(Haijachapishwa).*

Otunga, N., Odeo, I. I, & Barasa, L. (eds.) (2011). *A Handbook for Curriculum and Instruction*. Eldoret: Moi University Press.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1551

Owala, J. A. (2014). *Mitazamo Kuhusu Kiswahili Miongoni Mwa Wazungumzaji Wa Kijaluo-Kifani Cha Shule Za Msingi Katika Kaunti Ya Migori* (Doctoral dissertation, University of Nairobi).

Oxford, R.L. (1997). Cooperative Learning, Collaborative Learning, and Interaction: Three Communicative Strands in the Language Classroom. *The Modern Language Journal. Vol.81, No. 4, Special Issue: Interaction,Collaboration, and Cooperation: Learning Languages and Preparing Language Teachers. Wiley Publishers.*

Rosenthal, R., & Jacobson, L. (1968). *Pygmalion in the classroom: Teachers' expectations and pupils' intellectual development*. Holt, Rinehart and Winston.

Rutere, J. K. (2012). *Effects of teacher related factors on implementation of integrated Kiswahili curriculum in public secondary schools in Nkuene Division, Imenti South district, Kenya* (Doctoral dissertation, University of Nairobi, Kenya).

Stitt-Gohdes, W. L. (2001). Business Education Students' Preferred Learning Styles and Their Teachers' Preferred Instructional Styles: Do They Match?. *Delta Pi Epsilon Journal*, *43*(3), 137-51.

Tume ya Koech (1999). *Report of the Commission of Inquiry on the Education system in Kenya*. Nairobi; Government Printer Kenya.

Wambui, H. K. (2017). Tathmini ya matumizi ya vifaa vya kufundishia msamiati wa Kiswahili katika shule za msingi za umma, Kaunti ya Kisumu Mashariki, Kenya. *International Journal of Emerging Trends in Science and Technology*, 3(10)

Watson, M. (2003). *Learning to trust: Transforming difficult elementary classrooms through developmental discipline*. San Francisco: Jossey-Bass.

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.